

KISWAHILI

KARATASI YA 3

JANUARY /FEBRUARY, 2013

MUDA: SAA 2½

MTIHANI WA KUJISAJILI

BUNYORE-MARANDA (BUMA 1)

MAAGIZO

- a) Jibu maswali **manne** pekee.
- b) Swali la **kwanza** ni lazima
- c) Maswali hayo mengime matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani:Riwaya, Hadithi Fupi, Tamthilia na Fasihi Simulizi.
- d) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
- e) **Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa**
- f) **Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa maswali** yote yamo na **kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa**.
- g) Kumbuka kuchora jedwali la maswali uliyoyajibu juu ya karatasi yako ya majibu.

## **SEHEMU A: LAZIMA**

### **1. USHAURI**

Linatushangaza, twashangaa dhidi ya kushangaa!  
Kwa mangamizi ya kila leo.  
Tunayotekelzewa na kiumbe razini zaidi,  
Binadamu!

Hatuui sababu,  
Mzinga na mazega yetu kuteketezwa,  
Yetu asili kurinwa kwa mababu na waritimba,  
Binadamu wasiojua madhila yetu,  
Kudamka kutafuata nekta, na kukesha kulinda mzinga!  
Lakini kinachotushangaza, twauliza: mwatuchomeani?

Twafedheheka jamani!  
Masaibu ya tajiri,  
Tajiri mwema kuwatahirisha wasio na faida  
Badala ya wakatilia moto daraja la fanaka,  
Wasijue kesho, kesho kutwa, mtondo.....watavuna wapi?  
baada ya kutuangamiza, sie vitega chumi vyao.

Tuma haki, kama nyinyi,  
Ya kuwaona watoto wetu na wetu vijukuu,  
Wakikua na kufaidi, jasho letu wazazio,  
Ingawa hili halijawa faradhi,  
Ila kwa mapenzi yenu ya dhati.

Kumbuka binadamu,  
Hata sisi tuna hisia, tuisichomwe,  
Japo wajinga, tunayo manufaa,  
Sie hatuwahi, mbona nyie?  
Na safari yetu sote, japo njia tofauti.  
Twende polepole!

### **Maswali**

- a) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)
- b) Eleza muundo wa shairi hili. (alama4)
- c) Taja na ueleze tamathali za semi mbili zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
- d) Huku ukitoa mifano mwafaka eleza aina mbili za idhini ya mtunzi zinavyojitokeza tungono (alama 4)

- e) Oneysha umuhimu wa matumizi ya vihisishi katika shairi (alama 2)
- f) Andika ubeti wa pili katika lugha nathari. (alama 4)

### **SEHEMU B: UTENGANO**

#### **Jibu swali la 2 au 3**

- 2. Kutowajibika kwa wanaume ndiko kumekuwa chanzo cha mizozo na uozo wa maadili katika jamii. Thibitisha kwa kurejelea riwaya ya utengano (alama 20)
- 3. ‘Ah bibi we, kupeana ni kikoa. Nataka kwenda kumpa Yule karani wa viwanja, chai, yake, anifanyie mpango nikipate kele kiwanja.’
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
  - b) Taja na ufafanue mbinu za lugha zilizotumika katika nukuu hili. (alama 4)
  - c) Jadili kuwepo kwa swala la ‘chai’ katika jamii husika. (alama 12)

### **SEHEMU C: DAMU NYEUSI NA HADIDHI NYINGINE**

#### **Jibu swali la 4 au 5**

- 4. “Hadi lini ? hadi lini.....ataendelea kurudi nyumbani chakari na wimbo wake huu? Mwisho wa haya utakuwa lini, Ya Rabi?”
  - a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
  - b) Eleza tamathili za usemi mbali zilizotumika katika dondoo hili. (alama 4)
  - c) Fafanua madhara sita ya uchakari wa anayerudi nyumbani. (alama 6)
  - d) Ni mambo gani yaliyomfanya anayejiuliza maneno haya kurudhia hali hii (alama 6)
- 5. Jadili mbinu zifuatazo kifasihi katika hadidhi kikza
  - a) Jazanda (alama 4)
  - b) Majazi (alama 6)

### **SEHEMU D: TAMTHILIA NA FASIHI SIMULIZI**

#### **Jibu swali la 6 au 7**

#### **TAMTHILIA: MSTAHIKI MEYA-TIMOTHY M. AREGE**

- 6. Tamthilia ya MSTAHIKI MEYA inaa fiki yanayoendelea katika baadhi ya nchi za bara la afrika. Thibitisha (alama 20)

#### **FASIHI SIMULIZI**

- 7. a) Fafanua fani zifuatazo za fasihi simulizi (alama 6)
  - i. Ngano za mtanziko
  - ii. Mazingira
  - iii. Kifunga nyama
- b) Umeombwa kusimulia darasani mughani wa Fumo Liyongo, eleza namna utakavyofanikisha uwasilishaji wako. (alama 10)
- c) Je, ni vipi jamii ya kisasa inaendeleza Fasihi Simulizi (alama 4)